



Kumb. Na:TR20210920/01

MKUTANO MKUU NA UCHAGUZI WA TANRIKS 2022

Uongozi wa Tanriks unapenda kuwajulisha Diaspora Watanzania kuwa, Mkutano Mkuu wa Tanriks 2022 utafanyika Malmö tarehe 26 Machi 2022. Uamuzi huo umefikiwa baada ya mkutano wa Bodi ya Ushauri ya Tanriks uliofanyika tarehe 26 Septemba 2021. Mgeni rasmi ni Mhe. Balozi Grace Martin Olotu, Balozi wa Tanzania Nordic, Baltic na Ukraine na Mlezi wa Tanriks.

Kwa kuwa mkutano huo utakuwa na uchaguzi wa viongozi, Uongozi wa Tanriks unawakumbusha wanachama kulipa Ada zao ili waweze kutimiza haki zao kwa mujibu wa katiba ya Tanriks. Unaweza kulipa Ada yako kupitia Swish 1230227694 – [Tanzaniskariksförbundet](#), na kumjulisha Mtunza Hazina kwa simu +46760558079, au kulipa Ada yako kidigital kupitia link hii [Member Login – TANRIKS](#).

Kwa wale watakaohitaji msaada wa Tehama kukamilisha ulipaji wa Ada zao tunawaomba kuwasiliana na Mkurugenzi wa Tehama, Eng. Jonathan Kayumbo simu +46724511963 /kutuma barua pepe kwa admin@tanriks.com.

Taarifa hii ya awali ya Mkutano Mkuu inatolewa ili kuwawezesha Wanachama na Diaspora wengine kujiandaa mapema, kushiriki na kufanikisha Mkutano huo. Taarifa zaidi zitaendelea kutolewa ikiwemo jinsi ya kushiriki katika kuchaguliwa katika uongozi kwa kadri zinavyokamilika.

Tanriks inatanguliza shukrani kwa ushirikiano mkubwa mnaotupatia. Asanteni.

TANRIKS INAWALETA WATU WOTE PAMOJA

Elizabeth Pedersen

Elizabeth Pedersen

Mwenyekiti

Tanriks

17-12-2021